

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA



Mkuu wa TAKUKURU (M) Simiyu

S.L.P 306, Simiyu

Simu: (028) 2700374 Nukushi (028) 2700532

Barua pepe:rbcsimiyu@pccb.go.tz

Wavuti www.pccb.go.tz

19/06/2020

KORTINI KWA WIZI WA SHILINGI 880,000/-

JUNI 19, 2020

Afisa Afya wa Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi mkoani Simiyu, amefikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Bariadi akikabiliwa na mashtaka kumi na moja ya kusababisha wizi wa shilingi 880,000/- mali ya halmashuri ya wilaya ya Bariadi. Kesi hiyo namba 75 ya mwaka 2020, imefunguliwa leo tarehe 19.06.2020 na TAKUKURU kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Mshitaka.

Mbele ya Hakimu wa Mahakama hiyo, Mheshimiwa Mary Mrio, Mwendesha Mashtaka wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Mkoa wa Simiyu, Carson Nkya, mshitakiwa Jumanne Sudi Kisanka, alidaiwa kughushi nyaraka zinazoonesha kuwa watumishi Nane kila mmoja alilipwa shilingi 100,000/- na mtumishi mmoja alilipwa shilingi 80,000/- kinyume na vifungu namba 333, 335(1)(a) na 337 vya Kanuni ya Adhabu. Mshitakiwa pia ameshitakiwa kwa makosa ya kuiba akiwa mtumishi kinyume na vifungu namba 255 na 270 na kuharibu nyaraka kinyume na kifungu namba 342 vya kanuni ya Adhabu. Mshitakiwa anadaiwa kutenda makosa hayo Desemba 21, 2015.

Watumishi waliodaiwa kughushiwa saini zao na mshitakiwa na kulipwa shilingi 100,000/- kila mmoja ni Masuke Lonungu, George Mgata, John Stephano, Shenye Lugiko, George Epaphra, Naomi Elikana, Jilala Konga, na Agnes Magamla. Mtumishi Mpejiwa Shilatu anadaiwa saini yake kughushiwa na kulipwa shilingi 80,000/- Mshitakiwa amepata dhamana ambapo mdhamini alitakiwa kusaini bondi ya shilingi Milioni Mbili huku kesi itatajwa tena tarehe 9.7.2020

Imetolewa na:

ADILI ELINIPENDA

Mkuu wa TAKUKURU (M) Simiyu.